2) Mmiliki wa Jina la Biashara lazima awe na nambari ya utambulisho wa utaifa (NIN) inayotolewa na NIDA

**Hatua za kusajili jina jipya la Biashara**

1. Tembelea Mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao kwa anwani ya wavuti https://ors.brela.go.tz/ors au kwa kutembelea tovuti ya BRELA: www.brela.go.tz na chagua **"BUSINESS NAMES ONLINE REGISTRATION"**
2. Kama huna akaunti kwenye mfumo wa ORS, bofya **"Tengeneza Akaunti ya ORS"** na ikiwa una akaunti tayari, ingia kwenye mfumo kwa kutumia jina lako la mtumiaji na nenosiri.
3. Bonyeza **"Anza"** na kisha **"Huduma mtandao"**
4. Chagua **Jina la Biashara**
5. Katika **aina ya huduma,** chagua **"Usajili wa Jina Jipya la Biashara"** na kisha bofya **"Endelea"**
6. Katika **aina ya jina la biashara,** chagua aina. mfano **"binafsi"** na bofya **"Endelea"**
7. Katika Fomu ya Usajili, jaza sehemu zote zilizowekewa nyota (*) ya rangi nyekundu.
8. Kwa kila hatua, kumbuka bonyeza **"Hifadhi"** ili kuhifadhi taarifa zako ili kuepuka kupoteza taarifa
9. Katika sehemu ya Mwombaji, jaza Taarifa ya Uwakilishi (Mmiliki au mshiriki
10. Kama mwombaji anaweza kuboresha data katika ORS bofya kitufe **"anaweza kurekebisha taarifa kwenye ORS"**
11. Katika sehemu ya "Maelezo kuhusu jina la biashara", jaza Jina la Biashara.
12. Jaza taarifa zote zinazotakiwa katika sehemu ya "Ofisi ya kusajiliwa"
13. Katika sehemu ya "Shughuli ya Biashara", bofya Ongeza ili kuchagua shughuli zako za biashara / malengo kulingana na Uainishaji wa "ISIC Classification" toleo la nne
14. Katika sehemu ya "Umiliki", bofya "Ongeza" ili kuongeza maelezo na anwani ya mmiliki wa Jina la Biashara
15. Katika sehemu ya "Mmiliki wa akaunti ya benki," jaza taarifa ya watu ambao wataendesha akaunti ya benki ya biashara
16. Kwa sehemu ya "Wawakilishi," taja mtu ambaye anaweza kurekebisha taarifa katika mfumo wa ORS. Ikiwa Mmiliki / Washiriki wanaweza kurekebisha taarifa, chagua "Ndio au Hapana" ili kuwawezesha au usiwawezeshe kuwa na mamlaka ya kuwapa watu ambao wanaweza kurekebisha taarifa katika ORS, kisha kwenye eneo la "inawakilishwa mpaka", jaza kipindi ambacho mtu huyu anaweza kurekebisha taarifa na kisha bofya "Endelea"
17. Subiri "consolidated form" itengenezwe.
18. Pakua fomu, kisha piga chapa (print) , weka sahihi pamoja na tarehe.
19. Pakia fomu iliyofanyiwa "Scanning" na kisha bofya "Endelea"
20. Katika ukurasa wa malipo, chagua njia ya kufanya malipo na kisha bofya "Kuanza malipo". Nambari ya kulipia itazalishwa. Bofya kwenye kitufe cha "Angalia" au "Pakua" ili uone taarifa za malipo pamoja na maelekezo ya jinsi ya kufanya malipo.
21. Mara baada ya kufanya malipo, maombi yako yanawasilishwa kwa BRELA moja kwa moja kwa ajili ya kufanyiwa kazi

**NAMNA YA KUFUATILIA MAENDELEO YA MAOMBI YAKO**

Angalia upande wa kushoto ndani ya mfumo , bonyeza sehemu ya Maombi (Applications)
Tazama sehemu ya **"Imefanyiwa kazi?"** Kama ni **"Yes"** inammanisha ombi lako limeshughulikiwa hivyo bofya **"View"** kuangalia taarifa zaidi ikiwemo kuprint cheti.
Kama "Imefanyiwa kazi?" inasema **"NO"** na sehemu ya **"Hatua ya kazi"**:-

- Inasema **"Process and Enter Recommendation"** inamaanisha maombi yako BRELA na yanafanyiwa kazi.

Kama inasema **"Make Final Decision"**, inamaanisha Maombi yako hatua ya mwisho kufanyiwa maamuzi BRELA.

HUDUMA KWA WATEJA:
0735 331 001, 0735 000003, 0735 331 004

P. O. Box 9393, Dar es Salaam - Tanzania
Tel: +255 22 218 0139, 218 1344,
218 0113, 2180141, Fax: +255 22 218 0371
Email: usajili@brela.go.tz, ceo@brela.go.tz,
Web: www.brela.go.tz

BRELA
WAKALA YA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

# MUONGOZO WA USAJILI WA KAMPUNI KWENYE MFUMO WA USAJILI KWA NJIA YA MTANDAO (ORS) NA MSAADA WA HARAKA KWA KUANDIKISHA JINA JIPYA LA BIASHARA KATIKA MFUMO WA USAJILI KWA NJIA YA MTANDAO (ORS)

## MUONGOZO WA USAJILI WA KAMPUNI KWENYE MFUMO WA USAJILI KWA NJIA YA MTANDAO (ORS)

Kabla ya kusajili au kupata huduma kwenye mfumo wa usajili hakikisha umetimiza masharti yafuatayo:

1) Kufungua akaunti kwenye mfumo lazima kuwa na kitambulisho cha utaifa kutoka NIDA.
2) Kama ni MBIA kwenye kampuni lazima uwe na kitambulisho cha utaifa kutoka NIDA,
3) Kama ni mkurugenzi wa kampuni, lazima uwe na kitambulisho cha utaifa kutoka NIDA na namba ua utambulisho wa mlipa kodi (TIN) kutoka TRA.

KUMBUKA: Wasio watanzania wanatakiwa kuwa na namba ya hati ya kusafiria (Passport) ya nchi husika.

## HATUA ZA USAJILI

1) Tembelea mfumo wa usajili kupitia https://ors.brela.go.tz/ors au kupitia tovuti ya BRELA www.brela.go.tz na bofya **"LIMITED COMPANY ONLINE REGISTRATION"**

2) Kama huna akaunti kwenye mfumo, bofya **"Tengeneza akaunti ya ORS".** Kama una akaunti tayari bofya **"Huduma mtandao kwa watumiaji wasiosajiliwa".** Ingia kwenye mfumo kwa kuweka **Jina la Mtumiaji na Neno la siri (Nywila).**

3) Bofya **"Anza"** kisha chagua "Huduma mtandao".

4) Chagua **"Kampuni".**

5) Kwenye **"Aina ya huduma"** chagua **"Usajili wakampuni mpya"** kisha bofya **"Endelea"**

6) Kwenye aina ya kampuni chagua aina ya kampuni. Mfano **"kampuni ya faragha Imepunguzwa kwa hisa"** kisha bofya **"Endelea"**

7) Kwenye fomu ya maombi, jaza taarifa zote zinazotakiwa ambazo zimeweka **alama ya nyota nyekundu (*).**

8) Kumbuka kubofya kitufe cha **"Hifadhi"** kwa kila taarifa unayoingiza zisipotee.

9) Sehemu ya **"Mwombaji"** jaza **"Kauli ya uwakilishi" kama ni Mkurugenzi / katibu/ mwakilishi**

10) Kama mwombaji anaweza kubadili taarifa kwenye mfumo wa ORS, bofya **"Anaweza kurekebisha taarifa kwenye ORS".**

11) Sehemu ya **Kitambulisho** jaza **Tarehe ya Uhasibu** na **Jina la kampuni.** Kama uliomba kuhifadhi jina, jaza **Namba ya kuhifadhi.**

12) Jaza taarifa zote kwenye sehemu ya Ofisi ya kusajiliwa.

13) Kwenye sehemu ya **Shughuli ya biashara,** bofya **"Ongeza"** na jaza shughuli zote za biashara ambazo KAMPUNI inaakusudia kufanya kwa kufuata mfumo wa kimataifa wa orodha ya shughuli za kibiashara na huduma (ISIC Classification Ver 4).

14 Sehemu ya **WAKURUGENZI,** bofya **"Ongeza"** kisha jaza taarifa za wakurugenzi wa kampuni. Angalau wawili.

15) Sehemu ya **KATIBU wa mkampuni,** jaza taarifa za katibu wa KAMPUNI.

16) Sehemu ya **Mtaji wa KAMPUNI,** chagua aina ya mtaji wa kampuni kama ni **"Kawaida"** au **"Mwingine".**

17) Sehemu ya **Hisa za mtaji zilizotolewa,** weka **"idadi ya hisa zilizotolewa"** na **"thamani"** ya kila hisa

18) Sehemu ya **"Wanahisa au Shareholders"** bofya **"Ongeza"** na ingiza taarifa za wanahisa. Wasiopungua wawili.

19) Sehemu ya **Idadi ya hisa zilizoshikiliwa** chagua mwanahisa kutoka kwenye orodha sehemu ya **"Chagua mwanahisa kutoka orodha"** na **"Daraja"** kisha Bonyeza **"Add shareholder to the table below"**

20) Sehemu ya **Wawakilishi,** weka taarifa za wawakilishi (Watu wanaoweza kufanya marekebisho au mabadiliko kwenye mfumo wa ORS). Kama Wakurugenzi/Wanahisa wanaweza kufanya marekebisho, bofya **"Anaweza kurekebisha taarifa kwenye ORS"** kisha bonyeza kitufe cha "Endelea"

21) Mfumo utakupeleka sehemu ya kupakua na kupakia fomu na Malengo na Katiba ya Kampuni. Subiri **"Consolidated form"** kisha **ipakue, saini,** weka tarehe na scan fomu hii

22) Pakua **fomu ya maadili, saini** na **gonga mhuri** wa Kampuni.

23) Pakia **Consolidated form, fomu ya maadili (Integrity form), Malengo na Katiba ya Kampuni (Memorandum and Articles of Association).** Kisha bofya **"Endelea"**

24) Mfumo utakupeleka kwenye ukurasa wa kufanya malipo. Chagua aina ya njia unayotaka kufanya malipo.

25) pakua taarifa ya maelekezo y namna ya kufanya malipo na kisha fuata maelezo.

26) Baada ya kufanya malipo, maombi yako yatatumwa na mfumo kwa ajili ya kufanyiwa kazi BRELA na yatahama kutoka sehemu ya Orodha yangu kwenda **sehemu ya Maombi.**

## NAMNA YA KUFUATILIA MAENDELEO YA MAOMBI YAKO

Angalia upande wa kushoto ndanin ya mfumo, bonyeza sehemu ya **Maombi (Applicatioans)**
Tazama sehemu ya **"Imefanyiwa kazi?"** Kama nia **"Yes"** inamaanisha ombi lako limeshughulikiwa hivyo bofya "View" **kuangalia taarifa zaidi ikiwemo kuprint cheti.**
Namba ya cheti cha usajili wa kampuni ndiyo namba ya utambulisho wa mlipa kodi TIN hivyo tembelea ofisi ya TRA iliyo karibu nawe ili kupata cheti chako cha TIN.
kama **"Imefanyiwa kazi?"** inasema **"NO"** na sehemu ya Under "Hatua ya kazi'
Inasema **"Process and Enter Recommendation"** inamaanisha maombi yako BRELA na yanafanyiwa kazi.
Inasema **"Make Final Decision"** inamaanisha maombi yako hatua ya mwisho kufanyiwa maamuzi BRELA.

## MSAADA WA HARAKA KWA KUANDIKISHA JINA JIPYA LA BIASHARA KATIKA MFUMO WA USAJILI KWA NJIA YA MTANDAO (ORS)

Kabla ya kusajili Jina la Biashara, lazima uwe umekidhi vigezo vifuatavyo:-

1) Kufungua akaunti katika ORS lazima uwe na nambari ya utambulisho wa utaifa (NIN) inayotolewa na NIDA